## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 14/10/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

**MAHUDHURIO**

| | |
|---|---|
| 1. CONSATNTINE MTITI | Mwenyekiti wa muda |
| 2. SULEIMAN MPANJU | Katibu |
| 3. NEEMA ALIGAWESA | Mjumbe |
| 4. MARCO MASUE | Mjumbe |
| 5. MWL ROSE SANDI | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

| | |
|---|---|
| 1.. DKT BARNABAS MBWAMBO | Kwa taarifa |

**AGENDA:**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUSOMA NA KUIDHINISHA MUHTASAI WA KIKAO CHA TARHE 30/06/2021
3. YATOKANAYO NA MUHTASARI WA TAREHE 30/06/2021
4. KUSOMA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA MANUNUZI YA ROBO YA KWANZA 2021
5. KUIDHINISHA MABADILIKO YA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022
6. KUIDHINISHA MANUNUZI YA MIRADI YA MAENDELEO KUTUMIA UTARATIBU WA FORCE ACCOUNT.
7. KUFUNGA

**AGENDA NA 1: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha mwenyekiti ili afungue kikao na mwenyekiti alifungua mnamo saa 3;50 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe na kuwaeleza kuwa kikao hiki ni cha kawaida kwa mujibu wa sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011. na kuwasisitiza wajumbe kuwa watulivu na kutoa ushauri wao utakaowezesha kufanya maamuzi sahihi.

**AGENDA NA 2: KUSOMA NA KUIDHINISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 21/12/2021**

Mwenyekiti alimkaribisha katibu asome muhtasari wa kikao cha tarehe 30/06/2021 ambapo Muhtasari ulisoma na kufanyiwa masahihisho Kama ifuatavyo:

Agenda Na 1; Kufungua Kikao-***Wajumbe walishauri kuongezwa maneno kwenye msitari wa mwisho kama ifuatavyo:*** na kanunuzi za manunuzi za mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016.

Agenda Na 5: Kujadiili na kuidhinisha mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021- Kwenye aya ya pili neon ***ambapo alieleza*** liwe neno moja lisomeke ***Wenye***

**AGENDA NA 3: YATOKANAYO;**

Mwenyekiti aliwaomba wajumbe wapitie muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 30/06/2020 ili kuona kama kuna yatokanayo Wajumbe walipitia kwenye muhtasari huo,Wajumbe walitaka ufafanunuzi wa mambo mabalimbali na kutolewa majibu kama ifutavyo:

Agenda Na;4: **Taarifa ya manunuzi ya Robo ya nne;** Wajumbe walitaka kujua kwamba, wakati wa kikao cha kuondoka mkaguzi wa nje aliekagua mwaka wa fedha 2020/2021 alibainisha kuwa taarifa za ***lower level*** hazikuwasilishwa hivyo wamkataka katibu kutolea maelezo ya jambo hilo. Katibu alieleza kuwa Taarifa ya manunuzi iliyoandaliwa kwa Robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022 imehusisha taarifa za manunuzi za ***lower level.***

Agenda na 5: **Mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022:** Wajumbe walitaka ufafanuzi wa namna fedha zilizotolewa na serikali za ujenzi wa madarasa na vituo vya afya kama zimeunganishwa kwenye mpango huo kwani fedha zimekuja wakati mpango wa manunuzi ulishaidhinishwa. Majibu yalitolewa kuwa, mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 umehuishwa kwa kuingiza manunuzi ya miradi ya fedha za Covid19 na zile za tozo ya simu na taarifa yake imewekwa kwenye agenda namba 5 ya kikao cha tarehe 14/10/2021.

**AGENDA NA 4; KUJADILI NA KUIDHINISHA TAARIFA YA MANUNUZI YA ROBO YA NNE YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

Katibu aliwasilisha taarifa ya manunuzi ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:

A:Manunuzi ya Makao Makuu ya Halmashauri

Manunzui ya July yalikuwa ni Tsh 7,140,238.82
Manunuzi ya August yalikuwa ni Tsh 21,981,037.07
Manunuzi ya Septemba hayajafika mwisho yataunganishwa na taarifa ya robo ya pili.

**B.MANUNUZI YALIYOFANYIKA NGAZI YA CHINI.**

Kitengo cha manunuzi pia kilipokea taarifa za manunuzi kutoka ngazi ya chini (*lower level*) kama ifuatavyo:

i. Manunuzi ya Elimu msingi Jumla ya Tsh 91,555,227
ii. Manunuzi ya Elimu Sekondari jumla Tsh 5,582,560

**C. KAZI NYINGINE ZILIZOFANYIKA**

Mh mwenyekiti, kazi nyingine zilizofanywa na Kitengo cha manunuzi ni kama ifuatavyo:

i. Tumeratibu kikao cha Bodi ya Zabuni cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022
ii. Kussimamia na kutoa ushauri wa manunuzi mbalimbali ya Halmashauri ngazi ya wilaya na ngazi ya chini.
iii. Kitengo tumeendelea kujibu hoja za ukaguzi zinazojitokeza.

D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MANUNUZI 2021/2022

Katibu aliwasilisha kuwa, Halmashauri imetekeleza mpango wa manunuzi kwa kununua vifaa vya ujenzi, mafuta na magurudumu ya magari jumla ya kiasi kilichotumika ni Tsh **126,026,110.94.** (*Taarifa ya utekelezaji imeambatishwa nyuma)*

Wajumbe walipitia mchanganuo uliowasilishwa kwao wa manunuzi ya miezi husika na kujadili kwa kina na baada ya majadiliano walikubaliana kwa pamoja kuwa,kupitisha manunuzi hayo.***(mchanganuo wa manunuzi husika umeambatishwa nyuma ya muhtasari huu}***

**AGENDA NA 5 KUIDHINISHA MABADILIKO YA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

1. Katibu aliwasilisha mabadiliko ya mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo alieleza kuwa kwa sasa mpango utakuwa na Jumla ya Tsh 5,937,035,975.83 ikiwa ni manunuzi ya bidhaa, huduma,na kazi zisizo za ushauri. Alieleza kuwa sababu ya mabadiliko hayo ni kutokana na fedha zilizopokelewa na Halmashauri za ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za msingi na sekondari, ujenzi wa kituo cha afya Orkolili na nyumba ya mtumishi katika zahanati ya Roseline na ujenzi wa Shule ya sekondari ya Kata itakayojengwa Biriri. Wajumbe walijadili kwa kina na kuridhia mpango huo wa manunuzi uendelee kutumika kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**AGENDA NA 6: KUIDHINISHA MANUNUZI YA MIRADI YA MAENDELEO KUTUMIA UTARATIBU WA FORCE ACCOUNT.**

Katibu aliwasilisha manunuzi mbalimbali yanayotakiwa kufanyika ngazi ya "Lower Level" kwa kutumia njia ya Force Account kama ifuatavyo:

Ujenzi wa Kituo cha Afya Orkolili gharama yake ni Tsh 250,000,000/=
Ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika Zahanati ya Roseline 90,000,000/=
Umaliziaji wa Wodi mbili (wanawake na wanaume) katika Hospitai ya Wilaya Siha 152,469,750/=
Ujenzi wa Wodi mpya ya Wanawake katika Hospitali ya Wilaya Siha 140,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 katika shule ya msingi Neema 80,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 katika shule ya msingi Mwinuko 80,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madaras 4 katika shule ya msingi Mendai 80,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 katika shule ya msingi Namayani 40,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarsa 4 katika shule ya sekondari mathadi 80,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya Darasa 1 katika shule ya sekondari Magadini 20,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika shule ya sekondari Jitegemee 60,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika shule ya sekondari Karansi 60,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika shule ya sekondari Esinyari 80,000,000/=
Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika shule ya sekondari Sikirari 60,000,0000/=

Wajumbe walipitia orodha hiyo na kujadiliana na kina na kwa pamoja waliridhia utaratibu wa Force Account utumike kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya shule pamoja na vituo vya afya na Hospitali ya Wilaya.

**AGENDA NA 6: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na utulivu uliofanikisha kikao na alifunga kikao mnamo saa 5;55 Asubuhi.

Umethibitishwa.

.............................................

Constantine Mtiti
Mwenyekiti wa Muda

.............................................

Suleiman R.Mpanju
Katibu

Tarehe..15-11-2021.........................................